International Baccalaureate®
Baccalauréat International
Bachillerato Internacional

# MARKSCHEME
# BARÈME DE NOTATION
# ESQUEMA DE CALIFICACIÓN

## November / novembre / noviembre 2009

## SWAHILI / SOUAHÉLI / SUAHILI B

## Higher Level
## Niveau Supérieur
## Nivel Superior

## Paper / Épreuve / Prueba 1

*The answers given in this markscheme contain the essential information that candidates are expected to provide in order to gain full marks for each question.*

*Where appropriate, the information may be expressed in phrases other than those indicated, but full marks may only be awarded if all the necessary information is given.*

*Incomplete answers should be marked as directed.*

*Do not use half marks.*

*Unless otherwise indicated no marks are to be awarded or deducted for use of language: linguistic errors should only be taken into account if communication is severely impaired and the answer is incomprehensible to a normal speaker of the language.*

***Assistant Examiners are requested to wait until they are contacted by their team leader before beginning the marking (see the examiners instructions for further details).***

*Les réponses données dans ce barème de notation contiennent l'essentiel de ce qu'on demande aux candidats pour qu'ils puissent obtenir la note maximum pour chaque question.*

*Les réponses peuvent être formulées différemment mais la note maximum ne sera attribuée que si le contenu de la réponse est exact.*

*Les réponses incomplètes seront notées selon les indications données.*

*En aucun cas, des demi-points ou des fractions ne doivent être attribués.*

*À moins d'une indication spécifique, aucun point ne sera ni ajouté ni ôté pour l'utilisation de la langue : les erreurs linguistiques ne seront prises en considération que si elles nuisent sérieusement à la communication et rendent ainsi la réponse incompréhensible.*

***Les examinateurs assistants sont priés d'attendre d'être contactés par leur chef d'équipe avant de commencer leurs corrections (voir les instructions aux examinateurs pour de plus amples détails).***

*Las siguientes respuestas contienen la información esencial que los alumnos han de proporcionar para conseguir la máxima puntuación en cada pregunta.*

*En ocasiones, esta información puede expresarse de manera distinta a la indicada, pero para conseguir la máxima puntuación se han de mencionar todos los detalles requeridos.*

*Las respuestas incompletas deberán corregirse de la manera indicada en las instrucciones.*

*No utilice fracciones de puntos.*

*A menos que se indique lo contrario, no se deben añadir ni restar puntos por la calidad en el uso de la lengua: los errores lingüísticos sólo se tomarán en cuenta si la comunicación queda seriamente perjudicada o si la respuesta resulta incomprensible.*

***Se pide a los examinadores asistentes que esperen a ser contactados por su examinador líder de equipo antes de iniciar la corrección (para más información, refiéranse a las instrucciones para los examinadores).***

- ***One mark is allocated per question unless otherwise indicated.***
- ***Sauf indication contraire, chaque question vaut un point.***
- ***Cada pregunta vale un punto, a menos que se indique algo distinto.***

## SEHEMU YA A

### KIFUNGU A — MAWASILIANO KWA VITENDO KATIKA AFRIKA YA MASHARIKI

**1.** Si kizuri hasa kwenye utamaduni unaosisitiza watu kutowashika wengine bila hiari
*Neno lolote lilo na maana sawa na jawabu hili.*

**2.** Vitendo huonyesha heshima kwa watu wazima
*Neno lolote lilo na maana sawa na jawabu hili.*

**3.** (a) Kuangalia watu machoni *(kwa mpangilio wowote)* ***[Alama 1]***
(b) Kuweka mikono mfukoni ***[Alama 1]***
*Neno lolote lilo na maana sawa na jawabu hili.*

**4.** Kukonyeza jicho
*Neno lolote lilo na maana sawa na jawabu hili.*

**5.** Anayekitumia ni lazima awaangalie wale anaowataka wanyamaze
*Neno lolote lilo na maana sawa na jawabu hili.*

**6.** B, C *(kwa mpangilio wowote)* ***[Alama 2]***

**7.** A

**8.** B

**9.** H

**10.** F

**11.** E

**12.** C

**KIFUNGU A:** ***[Alama 14]***

**KIFUNGU B — FASIHI YA KISWAHILI KATIKA AFRIKA YA MASHARIKI**

**13.** K – inafanya kazi zile zinafanywa na kazi nyingine za fasihi kama vile riwaya na mashairi

**14.** S – inahusu ukombozi wa wanawake

**15.** S – zinaongea kuhusu maswala ya jamii

**16.** K – riwaya zilizoandikwa kwa fundi sana

**17.** K – ni mmoja kati ya walioandika riwaya nyingi

**18.** K – amechagia pakubwa katika fasihi ya Kiswahili/kazi zake zimetanda kote

**19.** Kazi zake zimetanda kote kwenye fani zote za fasihi– riwaya, tamthilia na mashairi

**20.** Zinajadili matukio mengi ya kijamii

**21.** Ameandika riwaya fupifupi za watoto

**22.** Waandishi wachanga/wapya/wanaokua
*Au maneno yeyote yanayoeleza dhana hii.*

**23.** B

**24.** B

**25.** A

**KIFUNGU B:** ***[Alama 13]***

**KIFUNGU C — NDOTO YA AMERIKA**

**26.** F

**27.** A

**28.** I

**29.** H

**30.** Huanza kutamani kwenda Marekani

**31.** Hakuwa ameota Ndoto ya Amerika

**32.** Mamake humcharaza viboko

**33.** Alifikiri Cairo ni mji katika Amerika

**34.** F

**35.** E

**36.** G

**37.** B, D *(kwa mpangilio wowote)* ***[Alama 2]***

**KIFUNGU C:** ***[Alama 13]***

**JUMLA SEHEMU YA A:** ***[Alama 40]***

## SEHEMU YA B

## KIFUNGU D — ATHARI ZA TEKNOLOJIA YA MAWASILIANO KATIKA JAMII ZA AFRIKA YA MASHARIKI

**Nia ya mawasiliano (Communicative purpose)**:
Barua rasmi kuhusu hasara za televisheni, simu na tarakilishi kwa jamii za Afrika ya Mashariki.

**A. Mawasiliano ya kitamaduni (Cultural interaction)**:

Nia ya swali hili ni kuandika barua rasmi kuhusu hasara za televisheni, simu na tarakilishi kwenye shughuli za mawasiliano katika jamii ya Afrika Mashariki. Mtahiniwa katika mtihani ni lazima aonyeshe kwa kinaganaga hasara za televisheni, simu na tarakilishi upande wa mawasiliano katika jamii ya Afrika Mashariki. Sajili inastahili iwe ya barua rasmi. Urasmi wa lugha hautahiniwi na unaweza kutumiwa tu iwapo makosa yanazuia maana inayonuiwa. Yafuatayo yanastahili kuwemo katika sajili husika: salamu, sehemu tatu za insha kwa mfano: mwanzo, kati na mwisho.

Ikiwa jibu la mwanafunzi halitaambatana na sajili mwafaka jibu halitapata zaidi ya alama 4.

**B. Ujumbe (Message)**:

Jibu mwafaka litatakiwa kutaja hasara za televisheni, simu na tarakilishi katika shughuli za mawasiliano katika jamii ya Afrika Mashariki. Maelezo kuhusu kunakili kwa kifungu yanastahili kuzingatiwa kwa makini. Unakili wa moja kwa moja wa sehemu fupi za kifungu haumaanishi "unakili usio rasmi", kunakili kwa sehemu ndefu au fupi bila "kuzitumia vema" (kuziingiza barabara kwenye jibu) ndiko kunakochangia "unakili usio rasmi".

Televisheni:
- Imeleta uzembe wa utendaji kazi kwa baadhi ya watu.
- Watoto badala ya kucheza hukaa ndani wakiangalia televisheni.
- Kukaa kwa muda mrefu kutazama televisheni huathiri afya za watu.
- Baadhi ya programu zinahimiza na kutukuza tabia mbovu miongoni mwa vijana na zimechangia pakubwa kwenye ongezeko la visa vya uhalifu katika jamii, ongezeko la dawa za kulevya, ulevi, mapenzi nje ya ndoa.
- Watu wameaga dunia kwa sababu ya kutenda maovu ambayo huyaona katika televisheni.

Simu:
- Zimetatiza kwa kiasi usiri wa watu. Ni rahisi kusikia watu wakiongea mbele ya watu wengine juu ya habari zao binafsi. Watu wote wanazipata habari zao za siri kwa urahisi.
- Ni rahisi kumwona mtu amegongwa kwa gari kwa sababu ya kuongea kwa simu njiani pasipo kufahamu kuwa kuna magari njiani.
- Watu wamekuwa wachache wa fadhila na siku hizi ni rahisi kusikia watu wakikipiga kelele kwenye simu pasipo kujali kuwa kuna wenzao.

Tarakilishi:
- Watu hutumia muda mrefu kwenye mtandao pasipo kufanya kazi yoyote ya maana.
- Nidhamu ya vijana imezorota kwa sababu ya wale wanayoyaona kwenye mtandao.
- Ongezeko la visa vya uhalifu na wizi.
- Vijana wengi wameanza kuacha shule.

**Sajili na Muundo (Register and Style)**:
Sajili inastahili iwe ya barua rasmi na inastahili iwe na maumbo yafuatayo: sehemu ya kwanza (anwani ya mwandishi na ya mhariri wa gazeti husika, tarehe, salamu na mintaarafu), sehemu ya kati (hatari za televisheni, simu za mkononi na tarakilishi) na tamati (sehemu ya mwisho-jina na sahihi ya mwandishi). Urasmi wa lugha hautahiniwi kirasmi na unaweza kutumiwa tu iwapo makosa yake yanazuia maana inayonuiwa.

**Criterion B**
Kupata alama 5 (uwelewekaji bora) wa criterion B, mtahiniwa lazima azingatie angalau hoja 6 ya zile zilizotajwa hapo juu.
Kupata alama 9 (uwelewekaji mwafaka) wa criterion B, mtahiniwa lazima azingatie angalau hoja 10 ya zile zilizotajwa hapo juu.

**JUMLA SEHEMU YA B:** ***[Alama 20]***

**JUMLA YA ALAMA:** ***[Alama 60]***